JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS – TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA KITETO

SHULE YA SEKONDARI ENGUSERO
S.L.P 33
KIBAYA-KITETO

Kumb. Na. ESS/BZMS/VOL.I/…… **25/03/2022**

Namba za simu
Mkuu wa shule: 0685229116/0752334693
Makamu mkuu wa shule:
Mzazi/mlezi wa mwanafunzi ……
S.L.P……..

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE (JOINING INSTRUCTIONS)
KIDATO CHA TANO 2022/2023 – MWAKA 2022

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka 2022 katika tahasusi ya …….. Shule ya sekondari **Engusero** ipo umbali wa kilometa 35 kusini mwa mji wa Kibaya. Usafiri unaotumika ni wa basi au Noah kutoka mjini unapatikana katika kituo cha mabasi kibaya, nauli ni shilingi 3000/=. Aidha kwa wale wanaopitia Dodoma na Morogoro usafiri wa moja kwa moja unapatikana na atashuka kijiji cha Engusero kabla ya kufika mji wa Kibaya.

Muhula wa masomo unaanza **mwezi Julai 2022.** Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni mapema mara tu baada ya maelekezo yatakayo tolewa na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za mitaa. (TAMISEMI)

Mambo ya kuzingatia

2.1 Sare ya shule

WASICHANA

a. Sketi ndefu-rangi blue bahari (mshono wa rinda box) jozi mbili na sharti ifikie vifundo viwili vya miguu.

b. Shati- rangi nyeupe mikono mirefu na tai rangi ya kitambaa cha sketi.

c. Viatu vyeusi visivyo na kisigino kirefu

d. Soksi nyeupe jozi mbili au zaidi.

e. Fulana ataipata shule kwa gharama atakazoelekezwa.

f. Sweta-blue bahari moja au zaidi shingo ya V

g. Hijabu (Juba na sio mtandio) nyeupe na nusu kanzu inaruhusiwa kwa wanafunzi waislamu tu.

h. Truck suit rangi ya kijivu yenye mistari wiwili myeupe kwenye mikono na miguu kwa matumizi baada ya muda wa darasani.

i. Pull neck rangi ya kijivu kwa mwenye matatizo ya kifua.

WAVULANA

a. Suruali- rangi ya blue bahari jozi mbili inchi 18. Isiwe ya kubana (vimodo)

b. Shati-nyeupe mikono mirefu jozi mbili

c. Viatu vyeusi vya kufunga kwa kamba

d. Soksi nyeusi

e. Fulana ataipata shule kwa gharama atakazoelekezwa.

f. Sweta-blue bahari moja au zaidi shingo ya V

g. Truck suit rangi ya kijivuyenye mistari wiwili myeupe kwenye mikono na miguu kwa matumizi baada ya muda wa darasani.

h. Tai rangi ya suruali

i. Mkanda mweusi wenye kifungio cha Kawaida
j. Pull neck rangi ya kijivu inaruhusiwa kwa ajili ya kujikinga na baridi

SHAMBA DRESS:

- Suruali au sketi rangi ya damu ya mzee ishonwe kama ilivyoelekezwa hapo juu
- Hijabu (Juba na sio mtandio) rangi ya chungwa na nusu kanzu na sketi (Sio suruali) inaruhusiwa kwa wanafunzi waislamu tu.

NB: Ni marufuku mwanafunzi kuvaa suruali zinazobana (vimodo),vikoti, makoti, vilemba, kofia, vizibao, bangili, mkufu na mapambo kama sehemu ya sare ya shule. Suruali chini ziwe na upana wa inchi 18, mbele iwe na rinda mbili (celebration) kila upande na mifuko miwili ya “cross” na nyuma iwe na mfuko mmoja. Aidha inatakiwa iwe na luksi sita za kuwekea mkanda.

2.2 **ADA NA MICHANGO YA SHULE**

a. Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi 20,000/= kwa mwanafunzi wa kutwa na shilingi 70,000/= kwa mwanafunzi wa bweni. Unaweza kulipa kiasi cha shilingi 10,000/= kwa mwanafunzi wa kutwa na shilingi 35,000/= kwa mwanafunzi wa bweni kwa muhula au kulipa ada yote kwa mara moja. Fedha hizo zilipwe kwenye Akaunti ya shule Na **50101100013 ENGUSERO SEC SCHOOL RECURRENT ACCOUNT**. Michango mingine ambayo siyo ya ADA ilipwe kwenye akaunti nambari **50103500046 ENGUSERO SECONDARY SCHOOL – SELF RELIANCE** katika Benki ya NMB (***Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip)***

b. Michango inayotakiwa kulipwa na kila mwanafunzi ni:-

i) Shilingi 10,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani

ii) .Shilingi 6,000/= kitambulisho pamoja na picha

iii) .Shilingi 20,000/= taaluma

iv) .Shilingi 20,000/= kuwalipa wapishi,walinzi na vibarua wengine

v) .Shilingi 2000/= nembo ya shule kwa ajili ya shati na track suit.

vi) Shilingi 5,000/=huduma ya kwanza,

vii) Tsh. 6000 bima ya afya.

viii) Shilingi. 23, 000 mitihani ya utamilifu (mock)

viii) Shilingi. 10,000 kukodisha godoro kwa muhula

ix) Shilingi. 5,000/= tahadhari na haitarejeshwa

c. Mahitaji ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-

i) Ream ya karatasi (A4) mbili (2) kwa mwaka, moja (1) kwa kila muhula

ii) Shuka jozi mbili rangi ya pink (wasichana) na light blue (wavulana) ,blanket 1 na foronya na chandarua

iii) vyombo vya chakula (sahani,bakuli,kijiko na kikombe)

iv) Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko kwa matumizi ya ofisi nan doo moja kubwa kwa matumizi ya ofisi.

v) Fyekeo - 1, Jembe - 1, Soft broom-1 na squeezer-1.

3.0 SEHEMU AMBAZO MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUONEKANA

Ni marufuku kuonekana sehemu zifuatazo:-

(a) Vilabu vya pombe (Bars, Night Clubs)

(b) Majumba ya Starehe (Cinema Halls, Disco Halls nk)

(c) Majumba ya kufikia wageni (Guest Houses)

(d) Nyumba za waalimu

4.0 **SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII:**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa mara baada ya kuripoti shuleni.

(c) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (Preparation).
(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
(f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa kufanya hivyo.
(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

4.1 **MAKOSA YANAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

(a) Wizi
(b) Uasherati/ubakaji/ulawiti/ushoga
(c) Ulevi wa aina yoyote
(d) Uvutaji wa bangi/utumiaji wa dawa za kulevya
(e) Makosa ya jinai
(f) Kupigana au kupiga
(g) Kuharibu mali ya mtu/ umma/fedha ya serikali kwa makusudi,
(h) Kudharau bendera ya taifa/viongozi wa serikali,
(i) Kuoa au kuolewa
(j) Kupata mimba/kumpa mwanafunzi wa kike mimba
(k) Kulala nje ya shule bila kibali cha Mkuu wa shule
(l) Kutoa mimba/kushiriki katika kutoa mimba
(m) Kutohudhuria vipindi vya darasani ikiwa ni pamoja na vipindi viwili (2) vya dini kwa wiki,

(n) Kugoma, kuchochea au kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu,
(o) Kukataa adhabu kwa makusudi,
(p) Kutoka nje ya shule bila sare ya shule na au bila kibali,
(q) Kumiliki simu ukiwa shuleni

5.0 **MAENEO YA KUFANYA KAZI**

5.1.0 **Mabwenini**

5.1.1 Kila mwanafunzi atapangiwa na mwalimu wa bweni eneo la kufanya kazi asubuhi na jioni baada ya saa za darasani

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla, ni jambo la lazima.

(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.

5.1.2 Hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi ya mwanafunzi atakayeacha kuhudumia eneo lake kikamilifu. Aidha kila asubuhi/jioni mwanafunzi anatakiwa kufanya usafi katika bweni na eneo lolote kama atakavyopangiwa na mwalimu/viongozi wake.

5.1.3 Ni **marufuku** kuwa bwenini wakati ambapo mwanafunzi anatakiwa kuwa darasani/miradi/michezo/Roll-check/Baraza nk.

5.2.0 **Darasani**

5.2.1 Wanafunzi wote wanatakiwa wawe madarasani

Kuanzia saa 1:30 – 4:00 asubuhi, 4:30asubuhi – 7:10 mchana, 7:20 – 8:40 mchana Saa 1:30 – 4:00 usiku

5.2.2 Darasa liwe safi (lisiwe na buibui, vumbi, karatasi nk) Mwalimu wa Darasa atakagua vyumba vya madarasa mara kwa mara. Kiongozi wa darasa na kiranja wahakikishe kila darasa ni safi.

5.2.3 Wakati mwanafunzi akiwa darasani anatakiwa afanye yafuatayo:-

(i) Mwanafunzi asipige kelele/asitoketoke darasani

(ii) Mwanafunzi aulize na kujibu maswali
(iii) Mwanafunzi afanye test/mazoezi/majaribio yote kwa uwezo wake wote. Kila mwanafunzi awe na daftari la mazoezi/test kwa kila somo.
(iv) Viti/madawati yapangwe kwenye mistari iliyonyooka
(v) Mwanafunzi **analazimika** kuhudhuria vipindi vyote kwa siku.
(vi) "Private Study" iliyopo kwenye ratiba ya siku hiyo ni **lazima** ifanyike darasani.

Ni marufuku kuhamisha kiti/dawati/taa/switch n.k. kutoka darasa moja kwenda mahali pengine.

Viongozi wa wanafunzi (monita na viranja) wahakikishe kwamba hakuna kifaa kilichohamishwa kutoka darasa moja kwenda mahali bila kibali cha mwalimu wa darasa

6.0 **CHAKULA**

6.1 Shule inaandaa Chakula kwa ajili ya Wanafunzi wote kila Siku. Kila Mwanafunzi **ni lazima** ale chakula hicho kinachoandaliwa na shule. Chakula kiliwe maeneo yaliyoruhusiwa tu, na ni marufuku kupeleka chakula Bwenini au mahali pengine popote nje ya eneo lililoruhusiwa bila KIBALI maalum. **Aidha,**

Hakuna Mwanafunzi anayeruhusiwa kutoka nje ya Mipaka ya Shule kwa ajili ya kutafuta Chakula wala hairuhusiwi mwanafunzi kuletewa chakula kutoka nje ya shule.

7.0 **UTAMADUNI NA MICHEZO**

7.1.0 **Michezo**

7.1.1 Shule ina michezo kama vile mpira wa miguu, wavu**,** pete, riadha, kuruka juu/chini na Sarakasi. Kila mwanafunzi ni **LAZIMA** ashiriki kikamilifu katika angalau mchezo mmoja. Utaratibu umeandaliwa na Mratibu wa michezo na Mwalimu Mwandamizi Malezi & Utamaduni.

7.1.2 Mwanafunzi ambaye hawezi kushiriki katika michezo hiyo awe na barua ya daktari na apewe kibali na Mkuu wa Shule.

7.1.3 Mashindano yatafanyika kila muhula na zawadi zitatolewa kwa washindi

7.1.4 Kutakuwa na Mchakachaka kila siku saa 11:45 asubuhi. **Ni lazima wanafunzi wote washiriki**

8.0 **SIKU ZA KUWATEMBELEA WANAFUNZI**

Baadhi ya wazazi wamekuwa wakifika shuleni kuonana na watoto wao kila wanapopenda. Hii imekuwa ikileta usumbufu shuleni ikiwa ni pamoja na kumpotezea mwanafunzi muda wa masomo. Siku ya kuonana na mwanafunzi ni Jumapili/Jumamosi ya kila mwisho wa mwezi kuanzia saa nne asubuhi hadi saa kumi na nusu jioni.

9:0 **MITIHANI**

Kila muhula wanafunzi wanafanya mitihani na matokeo kutumwa kwa wazazi. Mtoto wako ajitahidi asipate wastani wa alama **chini ya 50%**

Kama wewe Mzazi/Mlezi hupati matokeo ya mitihani ya mwanao (kila muhula), wasiliana na Shule haraka iwezekanavyo.
NB: Kila mwanafunzi aje na faili moja kubwa aina ya RADO kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu zake binafsi za taaluma.

10.0 **KURUDI SHULENI BAADA YA LIKIZO**

Ni jukumu la mzazi kuona kwamba mwanao anarudi shuleni angalau siku moja kabla ya siku ya kufunguliwa shule. Shule ikishirikiana na Bodi ya shule wana mikakati ya kuimarisha elimu ambapo mwanafunzi atakayechelewa kurudi kutoka likizo fupi au ndefu kwa wiki moja au zaidi itabidi **aje na mzazi/mlezi wake**. mwanafunzi ambaye hatakuja na **mzazi/mlezi hatapokelewa shuleni**. Aidha Mwanafunzi atakayechelewa siku moja hadi sita baada ya likizo fupi au ndefu **atapewa adhabu kali**.

Ukosefu wa ada hautakubalika kwamba ni sababu ya kuchelewa kuja shuleni.

11.0 **MENGINEYO**

11.1 **Muhimu kwa mzazi**

(i) Mchango **wowote** utakaotakiwa na shule ni lazima uwe na maandishi pamoja na Saini na muhuri wa Mkuu wa Shule. Kinyume cha hapo usimpe mwanao mchango ambao hauna barua.

(ii) Tabia na mwenendo wa mtoto wako akiwa likizo ni **jukumu lako** na tutafurahi sana kama utatuandikia kuhusiana na tabia ya mtoto wako alipokuwa likizo, mema/mabaya aliyofanya, ushauri uliompa mwanao pamoja na tarehe aliyotoka nyumbani kurudi shuleni. Maelezo haya yatatusaidia sana katika malezi ya mwanao.

(iii) Mzazi afuatilie sana utekelezaji wa vipengele namba 9:0 na 10:0 hapo juu.

(iv) **Mwanafunzi asije na simu ya mkononi (Cellular phone)**

(v) Mwanafunzi anayekuja hapa shuleni baada ya kusoma taratibu za shule hii **hategemewi kuvunja sheria/ kanuni na taratibu za shule** kwani akifanya hivyo ni kwa **makusudi** na **siyo bahati mbaya**

MWISHO

Karibu sana Shule ya Sekondari Engusero



M.MDUMA
MKUU WA SHULE

ORODHA YA VITABU UNAVYO WEZA KUJINUNULIA.

HISTORY.

1. A History of Modern Europe.
   1789 – 1981 By H. L. Peacock

2. Major events in the world History
- History paper 2 notes
- Advanced level F5 & F6
  By Gervas M. Zombe.

3. Major events in African Hist.
   By Jovitus F. Kamara Mweigage.
4. How Europe underdevelopment Africa.
   By Walter Rodney
5. Mastering African History in the world History up to 1945.
   By Mwl. Kato A. Gwampeewo.

ENGLISH.

English Advanced Learners' Dictionary Seventh/ Sixth Edition
By Macmillan Education L.td.

Novels. 1) Encounters from Africa
2) His Excellency the Head of State "Danny Safo"
3. A season of Waiting "David omowale"
4. A man of the people "Chinua Achebe"
5. The beautiful ones are not yet Born. "Ayi Kwei Arruali"
6. Divine providence. Severin N. Ndunguru"
7. The Rape of the pearl "Magola Nyago"
8. Vanishing shadows "Namige Kayondo"

LIST OF PLAYS.

1. Betrayal in the City – "Fancis Imbaga"
2. I will marry when I want "Ngung'o and Ngusi Wa Mirii"
3. The bride – "Austriri Bukenya".
4. Iwanda Magere – "Ohoit Omtatah"
5. An Enemy of the people. – Henrik J. Bsen.
6. Black Mamba. – "John Rugamba"

POETRY.

1. Selected poems – Institute of education
2. The wonderful surgeon and other poems. "Charles Mloka".

A student should purchase at least two books in each category of Novel, Plays and Poetry. A dictionary is Compulsory for proper achievements.

- A dictionary which you are advised to buy is the Oxford Advanced Learners Dictionary.

GEOGRAPHY

1. Physical Geography by D.T Msabila
2. Geography in Diagrams for Africa by R.B. Bunett
3. Practical Geography for Africa by John M. Pritchard
4. Human & Economic Geography (Advanced level paper 2) by D.T Msabila
5. Map Reading for East Africa by D. N. McMaster
6. Practical Geography (Map, Photo, statistics, survey& Research) for A. Level by Zisti Kamili
7. Research methology C.R.Kothari.
8. Principle of physical geography F.J Monkhouse

KISWAHILI

1. Nadharia ya Fasihi kidato cha tano na sita
2. Tahakiki – vitabu teule vya fasihi kidato cha tano na sita.
3. Riwaya
   - Usiku utakapokwisha – Mbunda Msokile
   - Kufikirika - Shaaban Robert
   - Mfadhili - Hussein Tuwa
   - Vuta N'kuvute – Shafii Adam Shafi
4. Tamthiliya
   - Kwenye Ukingo wa thim - Ebrahim Hussein
   - Morani – Emanuel Mbogo
   - Kivuli Kinaishi - Seif Mohamed
   - Nguzo Mama – Penina Muhando

5. Ushairi
   - Kimbuga - Haji Gora
   - Mapenzi Bora – Shaaban Robert
   - Chungu Tamu - Theobald A. Mvungi
   - Fungate ya Uhuru – Mohamed S. Khatibu
6. Nadharia ya lugha ya Kiswahili 1 kidato cha 5 na sita.
7. Tafsiri na Ukalimani
8. Historia ya lugha ya Kiswahili.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAISI
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KITETO
SHULE YA SEKONDARI ENGUSERO.

FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA SHULE NA MASHARTI YAKE.
FOMU HII IRUDISHWE SHULENI SIKU YA KURIPOTI MWANAFUNZI IKIWA IMEJAZWA KIKAMILIFU.

1. A: MWANAFUNZI.

Mimi ……. nimesoma kwa makini maagizo ya kujiunga na shule yako, pia sheria zake za shule kwa heshima na unyenyekevu mkubwa ninakubali/ninakataa nafasi hiyo na masharti ya shule na sheria zake kwa sababu

……..……
……
…….……..

Tarehe ……..... Sahihi ……

B: MZAZI/MLEZI.

Mimi ……...Mzazi/Mlezi wa ……. Ambaye amachaguliwa kujiunga na shule yako nimesoma maagizo na sheria zake. Ninakubali/ Ninakataa nafasi hiyo, ninaahidi/siahidi kumtimizia mtoto wangu mahitaji na maagizo yote ya kujiunga na shule kwa muda uliopangwa.

Aidha naahidi kushirikiana daima na uongozi wa shule katika kukuza, kumlea mtoto huyu kwa manufaa yake binafsi, wazazi na Taifa kwa ujumla.

Kama ninakataa (Eleza sababu) …….
……
……

Ahsante.

Jina na anuani ya Mzazi / Mlezi. ……
……

Sahihi ……... Tarehe ……

(Futa lisilohusika).

NB: Sehemu ‘B’ Isainiwe na Mzazi/Mlezi na si vinginevyo

THE MEDICAL EXAMINATION FORM.
(To be completed by the Government Medical Officer and be returned to the school on registration day).

Pupil's name in full ……..……

Blood count (Red and White Blood cells) ……

Stool Examination ……..……

Urine analysis: ……..……

Syphilis Test: ……..……

T.B. Test: ……

Ears: ……..……

Chest: ……

Spleen: ……..……

Abdomen: ……...……

Pregnancy test……

Additional information e.g. physical Defects or Impairment infections, clinic or Family Diseases etc.
.....

DECLARATION:

I certify that the above mentioned pupil is fit to pursue his/ her further studies.
(If do not fit please state it clearly)**.....**

Doctors Name**.....**

Doctor's signature**.....**

Date and Official Stamp**.....**